The University of Osaka Institutional Knowledge Archive

| | |
|---|---|
| Title | Nini ndiyo ‘Lugha’ : Kuzingatia Tofauti baina ya ‘Lahaja’ na ‘Kiswahili Sanifu’ Visiwani Zanzibar |
| Author(s) | Takemura, Keiko |
| Citation | スワヒリ＆アフリカ研究. 2018, 29, p. 167-187 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/69822 |
| rights | |
| Note | |

*The University of Osaka Institutional Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

The University of Osaka

# Nini ndiyo 'Lugha'

## - Kuzingatia Tofauti baina ya 'Lahaja' na 'Kiswahili Sanifu' Visiwani Zanzibar -[1)]

TAKEMURA Keiko

## 1. Haja ya Kuzingatia Uhusiano baina ya 'Lahaja' na 'Kiswahili Sanifu'

Tarehe 1 mwezi wa kwanza, mwaka 1930 Kamati ya Lugha (Kiswahili) ya Makoloni ya Uingereza (Interterritorial Language (Swahili) Committee)[2)] ilianzishwa kwa ajili ya 'kusanifisha na kukuza Kiswahili' katika makoloni ya Uingereza yaani Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar. Kamati hii iliamua 'lahaja ya msingi ya Kiswahili Sanifu' na kusambaza 'Kiswahili Sanifu'. Tangu wakati huo zaidi ya miaka 80 na kitu imepita tayari, Kiswahili sasa hivi ni 'Lugha ya Taifa' na 'Lugha Rasmi' huko Kenya na Tanzania. Na isitoshe, nchini Tanzania Kiswahili ndiyo lugha inayotumika na inayoeleweka zaidi ingawa katika nchi nyingi za Afrika hali ni tofauti kabisa kama vile lazima watumie Kiingereza ama Kifaransa kuwa lugha rasmi. Nchini Tanzania tangu miaka ya 1960 inaendelea kujadiliwa tena na tena kama Kiswahili kiwe lugha ya kusomeshea katika elimu ya kati na ya juu badala ya Kiingereza, lakini bado hali yenyewe haijabadilika. Na isitoshe hali imekwenda kinyume chake, yaani, siku hizi katika elimu ya msingi vilevile baadhi ya shule zinatumia Kiingereza badala ya Kiswahili kwa sababu kuna maoni yaliyoegemea sana juu ya kukithamini zaidi Kiingereza kuliko Kiswahili, ingawa vipengele vingi mno vya maisha ya kila siku kama katika siasa, uchumi, elimu, vyombo vya habari/mawasiliano n.k. vinaendeshwa kwa Kiswahili. Kwa hivyo inasemekana kwamba hadhi ya Kiswahili imekuwa kubwa sana nchini Tanzania kama lugha nyingine yoyote hata Kiingereza haiwezi kutekeleza kufanya kazi zake Kiswahili.

Lakini kuhusiana na mchakato wa kuanzisha Kiswahili Sanifu kumekuwa na mijadala ya mara kwa mara, hasa haki au uhalali wa kamati ile tuliyoitaja juu imetiliwa shaka (宮本 1982, 1989, 1990). Wengine wamesema, "Kiswahili Sanifu kimetengana kabisa na Kiswahili cha kiasili kinachozungumzwa na Waswahili, kimekuwa lugha mpya inayofuatana na sarufi ya Kiingereza".

---

[1)] Makala hii asili yake ni makala ya Kijapani iliyomo katika kitabu kinachoitwa *Gendai Africa no Shakai Hendoo - Kotoba to Bunka no Dootai Kansatsu* (kilichapishwa na Jinbun-Shoin, mwaka 2002) kilichohaririwa na Prof. Miyamoto Masaoki na Prof. Matsuda Motoji. Mara hii mwandishi wa makala ya Kijapani yaani mimi mwenyewe nimeitafsiri kwa Kiswahili.

[2)] Makao makuu ya kamati hii yaliwekwa Dar-es-Salaam, Tanganyika. Baadaye mwaka 1942 yalihamishiwa huko Nairobi, Kenya, halafu mwaka 1952 yakahamishiwa Makerere, Uganda. Halafu baada ya miaka 10 ikahamishiwa Mombasa, Kenya, na mwaka 1963 yalirudishwa tena Dar-es-Salaam. Mwishowe, kuanzia mwaka 1964, ilibadilishwa upya kabisa na kuwa taasisi moja ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, iliyoitwa 'Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili'.

Ilipoanzishwa Kamati ya Lugha (Kiswahili) ya Makoloni ya Uingereza, hapakuwapo hata na Mswahili mmoja miongoni mwa wanakamati, na ilipochaguliwa 'lahaja ya msingi ya Kiswahili Sanifu' nguvu za mishonari zilizokuwako Afrika ya Mashariki zilikuwa kubwa mno (竹村 1993:48-50), haiwezekani kukanusha maoni kama 'Kiswahili ni lugha iliyoundwa na shinikizo la nchi za nje'. Lakini hata hivyo, ukipenda au usipende, nchini Tanzania Kiswahili Sanifu ndiyo lugha iliyowaunganisha wananchi wakati nchi yenyewe ilipotaka kuwa 'taifa la kisasa'. Na tena imetajwa na kuthaminiwa kama hivi:

> Mtu akiongea Kiswahili chake mwenyewe yaani kama lahaja moja ya Kiswahili popote pale panapozungumzwa Kiswahili, kwa bahati mbaya inawezekana kuwa wengine wanaoongea Kiswahili kingine hawakifahamu hicho chake. Lakini Kiswahili Sanifu, lugha iliyozaliwa kwa ajili ya taathira ya siasa ya ukoloni, kinaweza kuwafanya watu wote wanaosema Kiswahili wafahamiane na kuvibadilisha kidogokidogo Viswahili vingine na kuvijumuisha (カルヴェ 1996:58).

Kiswahili kilitambulikana kama 'lugha ya cheo chini' kuliko Kijerumani wakati wa ukoloni wa Ujerumani na kuliko Kiingereza wakati wa ukoloni wa Uingereza (竹村 1993:39-41)[3], na tena hata hivi sasa hadhi ya Kiswahili haionekani kuwa ya juu kuliko Kiingereza nchini kote, lakini inasemekana kwamba kwa ajili ya Kiswahili Sanifu yaani mazao ya ukoloni yamefanya kazi kama kukifanya Kiswahili kitambulikane kuwa 'Lugha ya Taifa'.

Sasa tuangalie kwa makini 'lahaja' iliyokuwa msingi wa Kiswahili Sanifu ni ipi. Kama tulivyotaja tayari, wakati wa kuanzisha Kiswahili Sanifu mishonari kadhaa zilipigania kama lahaja ipi iwe msingi wa Kiswahili Sanifu. Mwishowe, Kiunguja-Mjini kilichoteuliwa na Mishonari ya UMCA ndicho kiliteuliwa kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu kwa kukishinda Kimvita kilichoteuliwa na Mishonari ya CMS[4]. Baada ya hapo, wakati Kiswahili Sanifu kiliposanifishwa, lugha hii ilibadilishwa kiasi cha kuambiwa kama "sarufi ya Kiswahili Sanifu imekuwa kama ya Kiingereza, hata kimofimu na kisintaksia, lugha hii imekuwa kama Kiingereza. Sura ya kiasili ya msingi wake Kiswahili Sanifu yaani lahaja ya Kiunguja-Mjini imeanza kufutika" (Maganga 1983:96)[5].

---

[3] Katika makala ya Mazrui na Mazrui (1995:9), juu ya cheo cha Kiswahili wakati wa ukoloni wa Ujerumani imetajwa hivi. "Hadhi ya Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano ilikuwa si moja tu. Kwa upande mmoja Kiswahili kilikuwa njia iliyounganisha watu na kuwafanya wawasiliane, lakini kwa upande mwingine kilikuwa 'lugha ya kati' ambayo iliwekwa katikati baina ya lugha ya watawala yaani 'lugha ya juu' na lugha za makabila yaani 'lugha ya chini'."

[4] Katika makala ya Miyamoto (1989:154) inaelezwa kwa makini juu ya hali halisi ya Kiunguja-Mjini.

[5] Katika makala ya Miyamoto (1989:157-161) ilitajwa mifano kadhaa ya 'mabadiliko' hayo ya 'hali halisi ya kiisimu ya kusanifisha Kiswahili'.

Je, kwa sasa hicho Kiunguja-Mjini kina thamani gani? Japo kimetambulikana kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu, kwa vyovyote vile hicho ni 'msingi' tu si 'Kiswahili Sanifu chenyewe', basi kinaonekana kuwa mojawapo ya 'lahaja' kama lahaja nyingine? Au inasemekana kuwa lahaja hiyo ina hadhi kubwa kuliko lahaja nyingine zote?

Mwanzoni, tuhakikishe kwamba 'lahaja' za Kiswahili zimechambuliwa vipi. Kwa mujibu wa makala ya Mkude (1983:67-68) tunajua kuwa lahaja za Kiswahili zimechambuliwa na Stigand (1915), Bryan (1959), Polomé (1967), Heine (1970), Chiraghdin (1977) n.k. Kutokana na kazi hizo, ingawa kuna tofauti kidogo ya njia ya kuchambua, takriban kazi zote zimesema kuwa idadi ya lahaja za Kiswahili ni kati ya 16 na 20. Kazi nyingine imesema kuwa kuna 'vilahaja' vya lahaja moja moja. Lakini "inajulikana kwamba ni vigumu sana kutofautisha 'lugha' na 'lahaja'" (Nurse & Hinnebusch 1993:37). Romain ameeleza "wakati tunapotaka kuhakikisha kwamba 'hii ni lugha' ama 'hii ni lahaja', kipimo cha kiisimu hakina msingi madhubuti, bali ni muhimu sana upande wa kijamii" (ロメイン 1997:14) kwa kuonyesha mifano ya hali ya Ulaya ambamo dhana za 'lugha' na 'lahaja' ndimo zilimozaliwa. Kusema la kweli hatuwezi kutofautisha 'lugha' na 'lahaja' kwa ukamilifu, kawaida tunabahatisha tu kwa kufuatana na mambo ya kijamii, yaani utambulizi kama 'hii ni lugha' ama 'hii ni lahaja' unategemea si sura ya kiisimu bali sura nyingine kabisa.

Kwa kawaida, wakati inapoamuliwa kutayarisha 'lugha sanifu' ifanye kazi kuwa 'lugha ya taifa', 'kilugha' ama 'lahaja' inayochaguliwa kuwa msingi wake inapata nguvu na haki kubwa ya kitaifa. Kwa sababu lugha hiyo inatakiwa kutumiwa katika vipengele vingi kama elimu, siasa, vyombo vya mawasiliano, uchumi, n.k., na kinyume chake lugha nyingine zote zisizochaguliwa hazitakiwi kutumiwa hata kidogo kirasmi. Hali hii imekuwa wazi tukiangalia hali halisi ya wakati wa kutayarisha 'Kijapani Sanifu'[6]. Lakini nchini Tanzania haiwezekani kusema kwamba 'lahaja' iliyokuwa msingi wa Kiswahili Sanifu haikupata nguvu na haki kubwa kuliko lahaja nyingine yoyote wala lugha nyingine yoyote.

Imeshaonyeshwa katika makala na vitabu mbalimbali kwamba kufuatana na upanuzi na ukuzaji wa Kiswahili kilichochaguliwa kuwa 'lugha ya taifa', pahala pa kutumia lugha nyingine zote za kienyeji yaani lugha zaidi ya 120 pamekuwa finyu sana sana, hata ziko lugha kadhaa ambazo baadaye zitakosa kabisa wasemaji wake[7], kwa hivyo wakati tunapoangalia hali ya lugha za Tanzania ni mada kubwa na muhimu 'uhusiano baina ya Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji'. Lakini katika majadiliano ya mada hiyo, kawaida kinachotiliwa umuhimu ni Kiswahili kinachotumiwa na kufahamiwa takriban nchini kote, yaani Kiswahili Sanifu. Na isitoshe, 'Kiunguja-Mjini' kilichosimuliwa kuwa ndicho msingi wa Kiswahili Sanifu hakitazamwi vizuri wala hakiwi mada ya kujadiliwa. Kwa maneno mengine, watu wanakiona Kiswahili kama 'lugha

[6] Uangalie kwa makini marejeo kama イ 1996, 長 1998, 安田 1999.
[7] Uangalie kwa makini tanbihi za 1) na 2) katika marejeo ya 竹村 1999:18-19.

moja'. Je, sasa tufikirie 'lugha moja' ni nini.

Mimi mwandishi mwenyewe ninatarajia kufafanua uhusiano baina ya lahaja iliyochaguliwa kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu na lahaja nyingine. Na tena, lazima tujadiliane kuwa zipo au hazipo taathira za Kiswahili Sanifu juu ya lahaja nyingine na kinyume chake yaani taathira za lahaja nyingine juu ya Kiswaili Sanifu. Hivi sasa inatambulikana kuwa kama lahaja nyingine zote zimeshajumuishwa katika Kiswahili Sanifu. Lugha yenye nguvu kubwa sana za kijamii na kiuchumi (kwa hapa Kiswahili Sanifu) na lugha yako mwenyewe unayotumia (kwa hapa lahaja fulani) ikiwa tofauti, hata usipolazimishwa, unaweza kubadilisha lugha unayotaka kutumia iwe Kiswahili Sanifu badala ya lahaja yako mwenyewe. Sasa lazima tuhakikishe kuwa hali hiyo imetokea au la baina ya Kiswahili Sanifu na lahaja nyingine.

Ili kufafanua jinsi wasemaji Kiswahili kama lugha ya kwanza (wengi wanaoishi katika mwambao wa Afrika ya Mashariki na visiwani) wanavyokitambua Kiswahili Sanifu, nilifanya utafiti wa mtazamo juu ya lugha huko visiwani Unguja na Pemba[8)]. Kutokana na matokeo yake, imefahamika kwamba istilahi yenyewe 'Kiswahili Sanifu' inatumiwa miongoni mwa wasomi wa elimu ya juu tu, na tena, watu wa kawaida hawajui dhana ya 'lugha sanifu' wala wanazisifu lugha zao (= lahaja zao). Kwao wao 'usanifu' ni 'usemaji lugha ambao mtu yeyote anaufahamu na ni wa kupendeza', kwa hivyo hawakutanabahi wala kutambua kuwa Kiswahili Sanifu ni lugha ya kutawala iliyotayarishwa na taifa (竹村 1999:12).

Katika makala hii, kwa kupitia uchambuzi wa tafiti kadhaa nilizofanya, tutajadili kuhusu hali ya kuwasiliana lahaja kwa lahaja, uelewa wa lugha wa wasemaji lahaja hasa taathira inayotokana na Kiswahili Sanifu. Kwa kazi hiyo tunatarajia kuhakikisha kwamba 'Kiswahili' ambacho kinaonekana kama 'lugha moja' kwa kweli ni 'mfululizo wa lahaja (dialect continuum)'. Na kazi hii iwe hatua ya kwanza ya kujibu swala langu mwenyewe kama "nini ndiyo 'lugha'".

## 2. Tofauti baina ya 'Lahaja': 'Tofauti ya Msamiati', 'Mipaka Inayoruhusiwa ya Kufanya Ndoa' na 'Mtazamo juu ya Lugha'

### 2.0 Maelezo ya Jumla ya Utafiti

Ili kubainisha taathira ya Kiswahili Sanifu juu ya 'lahaja', hali halisi ya kuwasiliana lahaja kwa lahaja, hali halisi ya kutumia lugha kwa wasemaji-lahaja na mtazamo wa wasemaji-lahaja juu ya lugha , nilifanya utafiti unaohusiana na tofauti ya msamiati, mipaka inayoruhusiwa ya kufanya

---

8) Utafiti huu uliendeshwa na bajeti ya kirasmi ya Wizara ya Elimu na Sayansi. Jina la mradi ni: Kuunda Eneo la Kiutamaduni na Miundo ya Kikabila Inayozalishwa na Lugha ya Mawasiliano ya Afrika ya Mashariki (Kiongozi: Prof. Miyamoto Masaoki). Utafiti huu wenyewe ni wa mwaka wa pili wa mradi huu. Nilifanya utafiti huu visiwani Unguja na Pemba kutoka tarehe 20 mwezi wa 7 mpaka tarehe 1 mwezi wa 9 mwaka 1997.

ndoa na mtazamo wa wasemaji-lahaja juu ya lugha katika Wilaya ya Kasikazini ‘A’ (WK) na Mjini Unguja (ZT). Juu ya tofauti ya msamiati, nilifanya utafiti huko ZT na katika vijiji vinane vya WK, hasa nilikusanya msamiati wa maneno 138 kama maneno ya wanyama, mimea, samaki, viumbe wa baharini, vifaa kadhaa vya nyumbani, n.k.[9] Niliwaomba wahojiwa wataje maneno wanayotumia zaidi kwa kawaida. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kuhakikisha uchambuzi uliofanywa na kazi nyingine za zamani ni sawa au la, na kufafanua kwamba taathira za umri na mahali walipozaliwa wazazi zinaonekana kwenye maneno wanayotumia wahojiwa au la.

Juu ya mipaka inayoruhusiwa ya kufanya ndoa tulifanya utafiti wa kuwauliza wahojiwa ana kwa ana kwa kutumia maswali ya jedwali la 1 katika WK[10]. Huko WK wakati nilipoanza kufanya utafiti mwaka 1998, barabara kuu ilikuwa inajengwa baina ya ZT tangu miaka 15 iliyopita, mwaka 1998 barabara hiyo ilikuwa imejengwa tayari mpaka kijiji cha Kidoti. Wakati nilipofanya utafiti ilikuwa bado inahitajika muda ili kujenga barabara hiyo mpaka kijiji cha Nungwi yaani Kaskazini kabisa ya kisiwani, hata hivyo, daladala zilikuwa zinakwenda na kurudi mara kwa mara kila siku mpaka Nungwi. Kutokana na hali hiyo, ilikuwa inakisiwa kwamba kabla na baada ya kujengwa barabara hii kuu kuna tofauti ya kiasi cha kwenda na kurudi watu mpaka ZT.

<Jedwali la 1> Maswali juu ya mipaka inayoruhusiwa kufanya ndoa baina ya wasemaji-lahaja za Kiswahili

| |
|---|
| 1. Umezaliwa wapi na unasema lugha gani / lahaja gani (Kiswahili cha wapi)? Utaje kwa zamu ya kuongea vizuri. |
| 2. Mwenzi (mke / mume) amezaliwa wapi na anasema lugha gani / lahaja gani (Kiswahili cha wapi)? Utaje kwa zamu ya kuongea vizuri. |
| 3. Ulikutana / Ulijuana vipi na mwenzi wako mara ya kwanza? Na mpaka kuoana kulikuwa na mchakato gani? |
| 4. Wakati mlipooana, ulitanabahi kuwa Kiswahili chako na chake mwenzi ni tofauti? Ikiwa ulitanabahi hivyo, tofauti ndiyo nini? Na ilitokea matatizo kutokana na tofauti hiyo? |
| 5. Mtoto / Watoto wanasema lugha gani / lahaja gani (Kiswahili cha wapi)? Kiswahili chao kimeanza kutofautiana na Kiswahili chako mwenyewe? |
| 6. Kabla na baada ya kujengwa barabara kuu, je, mipaka inayoruhusiwa kufanya ndoa imetofautiana? Ikiwa ni hivyo, kwa sababu gani? |
| 7. Umepata elimu shuleni? Ikiwa umewahi kupata elimu shuleni, Kiswahili cha shuleni na Kiswahili chako mwenyewe kimetofautiana? |
| 8. Unajua Kiunguja-Mjini? Ikiwa unajua hicho, umejua vipi? Unaongea hicho? Watoto wenu je, wanaongea? |

Halafu, mpaka ilipokuwa Tanzania kwa kuungana na Tanganyika mwaka 1964, wakazi wengi wa visiwani hawakuwaamini watu wa bara, na tena baina ya visiwa viwili pia kulikuwa na matatizo, Wazanzibari walikuwa wanawaonea Wapemba na kinyume chake pia. Wakati huo kuoana na watu wa ‘nje’ kuliepushwa kabisa, basi, inawezekana kukisia kuwa hata lugha pia zilikuwa hazitoki ‘nje’ wala haziingii ‘ndani’ ya vijiji, zinahifadhiwa vizuri. Kwa hivyo, ikiwa sasa mipaka inayoruhusiwa

[9] Utafiti huu pia ni wa mradi nilioutaja katika tanbihi ya 7, na ni wa mwaka wa tatu. Katika WK nilifanya utafiti kuanzia tarehe 16 mpaka 27 mwezi wa 9 mwaka 1998 na katika ZT kuanzia tarehe 9 mpaka 13 mwezi wa 9 na kuanzia tarehe 25 mpaka 30 mwezi wa 10 mwaka 1998.

[10] Utafiti huu pia ni wa mradi nilioutaja katika tanbihi ya 7, na ni wa mwaka wa tatu. Katika WK nilifanya utafiti kuanzia tarehe 15 mpaka 22 mwezi wa 10 mwaka 1998.

ya kufanya ndoa imepanuliwa, kuna uwezekano wa kuwasiliana kwa lugha/lahaja. Madhumuni ya utafiti huu, kwa hivyo, ni kufafanua hali ya kuhifadhi lugha/lahaja na mwendo wa kubadilika lugha/lahaja.

<Jedwali la 2> Maswali juu ya mtazamo wa wasemaji-lahaja za Kiswahili juu ya lugha (si yote)

| |
|---|
| 1. Unasema lugha gani / lahaja gani (Kiswahili cha wapi)? Utaje kwa zamu ya kuongea vizuri. |
| 2. Kwako wewe lugha gani ndiyo inayokusaidia zaidi katika maisha ya kawaida? |
| 3. Wazazi wako wanakutaka / walikutaka utumie lugha gani / lahaja gani (Kiswahili cha wapi) nyumbani kabla hujaenda shuleni? |
| 4. Wewe mwenyewe unamtaka / ulimtaka mwanao / wanao watumie lugha gani / lahaja gani (Kiswahili cha wapi) nyumbani kabla hawajaenda shuleni? |
| 5. Unakijua Kiswahili Sanifu? Ndicho Kiswahili gani? |
| 6. Unakijua Kiswahili Fasaha? Ndicho Kiswahili gani? |
| 7. Unaonaje nyumbani au majirani kinatumiwa (a) Kiswahili Sanifu (b) Kiunguja-Mjini? |
| 8. Unaonaje nyumbani au majirani kinatumiwa Kiswahili chako mwenyewe? |
| 9. Kiswahili chako mwenyewe ni lugha gani? Na kwa nini unaona hivyo? |
| 10. Kiswahili Sanifu ni lugha gani? Na kwa nini unaona hivyo? |
| 11. Kiunguja-Mjini ni lugha gani? Na kwa nini unaona hivyo? |
| 12. Ili wanao wahifadhi Kiswahili chako mwenyewe ulifanya / unafanya / unataka kufanya nini? |
| 13. Siku za mbele, hata ikiwa (a) Kiswahili Sanifu (b) Kiunguja-Mjini kitaingia ndani kwa ndani kijijini mwako, Kiswahili chako mwenyewe kitadumu daima? Kwa nini? |
| 14. Kwa mkaazi wa kijiji, ni muhimu kuongea Kiswahili chako mwenyewe katika kijiji chako? Ikiwa ni hivyo, kuna umuhimu wa kiasi gani? Na muhimu kwa nini? |
| 15. Unaweza kumwelewa mtu unayemwona mara ya mwanzo kuwa (a) aliyezaliwa kijijini mwako (b) aliyezaliwa sehemu nyingine mara moja? Kwa nini? |

Utafiti wa mtazamo juu ya lugha ulifanywa katika miji/vijiji kwa jumla 12 visiwani Unguja na Pemba kwa kutumia maswali ya jedwali la 2[11]. Madhumuni ya utafiti huu ni kufahamu hali halisi ya matumizi ya lugha ya wasemaji-lahaja na kufafanua wasemaji-lahaja wanatambua vipi Kiswahili Sanifu, wanaweka vipi thamani juu ya Kiswahili Sanifu na lahaja zao wenyewe, na mtazamo kama huo unaathiriwa na umri, elimu, aina ya kazi, pahala wanapokaa, n.k. au vipi.

## 2.1 Kuhifadhi Msamiati Vijijini

Kwanza tuhakikishe kuwa uchambuzi wa lahaja uliofanywa zamani unafuatana na hali halisi ya matumizi ya lugha ya wasemaji-lahaja ya sasa. Majibu ya watu 15 wa ZT wanaokaa hivi sasa mjini na hata waliowahi kukaa pahala pengine muda wa kukaa ZT ni mrefu zaidi kuliko pahala pengine, na majibu ya watu 30 ambao ni wanakijiji wa WK (Chaani, Kibeni, Mkokotoni, Moga, Nungwi, Kidoti, Matemwe, Mkwajuni), yanaonyesha matokeo yanayotuvutia.

Wakazi wote wa ZT wanajiona kuwa wanatumia Kiunguja-Mjini kwa kawaida, lakini hakuna maneno mengi ambayo watu 15 wamejibu majibu sawasawa. Na wakazi wa WK kabla ya utafiti

[11] Uangalie tanbihi ya 7.

walifikiriwa kuwa watajibu maneno ya Kitumbatu[12)] kinachozungumzwa katika eneo hili ama maneno ya vilahaja vya Kitumbatu, lakini baadhi ya watu walijibu maneno ya Kimakunduchi (kinaitwa Kihadimu/Kikae mara nyingine) kinachozungumzwa Kusini mwa kisiwani Unguja[13)]. Juu ya hayo unahitajika utafiti mwingine wa dhati, kwa hivyo ni swala litakalojibiwa baadaye.

Hapo chini tutaonyesha mifano 9 ya msamiati kwa kutumia picha. Hii mifano 9 inatuonyesha vidokezo vya kujua kama nguvu ya Kiswahili Sanifu ama Kiunguja-Mjini ya kuathiri lahaja nyingine za WK, tofauti kubwa sana ya matumizi ya maneno iliyomo ndani ya WK na vilevile iliyomo ndani ya ZT, na nguvu ya kuhifadhi maneno katika lahaja. Katika mabano baada ya jina la pahala inaonyeshwa idadi ya watu waliojibu.

### 2.1.1 Aina ya Wadudu

Hapa tuangalie maneno manne, yaani 'spider', 'flea', 'butterfly' na 'dragonfly'. Kwa Kiswahili Sanifu 'spider' ni 'buibui[14)]' na 'big spider' ni 'bui', lakini katika WK na ZT maneno haya mawili yametokea kwa mchanganyiko na tena kwa mara nyingi umbo la wingi wake ni tofauti. Halafu neno 'flea', bara kawaida neno 'funza' linatumika, na katika kamusi tunaliona neno hilo, lakini hakuna mtu hata mmoja anayetumia neno hilo katika utafiti. Neno 'butterfly' lina maneno kadhaa ya Kiswahili, na isitoshe, neno la Kiswahili Sanifu 'kipepeo (umoja)/vipepeo (wingi)' halikutajwa katika WK hata kidogo. Neno 'dragonfly' ni neno 'kereng'ende (umoja) / kereng'ende (wingi)' kwa Kiswahili Sanifu, lakini katika utafiti huu hakukuwa na mtu aliyetaja neno hilo bali yametokea maneno mengine kabisa.

---

[12)] Nurse & Hinnebusch (1993:11) wameeleza "lahaja hii inazungumzwa zaidi katika kisiwa cha Tumbatu kilichoko Kaskazini-magharibi ya kisiwa cha Unguja na katika mwambao wa ghuba ya Mkokotoni. Na Kusini mwa kisiwa cha Pemba na kisiwani Mafia na Kaskazini mwa Tanga, bara pia wako waliohama kutoka kisiwa cha Tumbatu. Kutokana na data za idadi ya watu za mwaka 1967 nchini Tanzania (kirasmi data hizo zilitolewa na serikali ya Tanzania mwaka 1971), pamoja na watu 6000 wa kisiwa cha Pemba na watu 1500 wa pahala pengine, kwa jumla wako wasemaji 53000 wa Kitumbatu." Kwa bahati mbaya hatujapata data nyingine mpya kuliko hii.

[13)] Uangalie kwa makini marejeo ya Chum (1994) juu ya msamiati wa Kimakunduchi. Katika kitabu hicho imetajwa kama hivi: "Kamusi hii imehaririwa kwa madhumuni maalum. Kwanza, tunawataka watu wa kizazi kijacho wahifadhi maneno ya asili yao. Wanaanza kuwasiliana na watu wa sehemu nyingine na matumizi ya maneno ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho yameanza kubadilika, basi, siku za mbele hali hii itazidi zaidi. Lazima tusikose msamiati wa Kimakunduchi hasa. ⋯ Kimakunduchi kinasemwa katika Mkoa wa Kusini hasa Pete, Jozani, Kitogani, Bwejuu, Paje, Jambiani, Mungoni, Muyuni, Kizimkazi, Kibuteni, Mtende na Makunduchi. Watu wanaokaa katika vijiji hivi wana lafudhi inayofanana sana. ⋯ Watu wa Makunduchi wakikutana wao kwa wao wanasema Kimakunduchi, wakikutana na wanaotoka sehemu nyingine wanasema lugha sanifu" (Chum 1994:112).

[14)] Huko visiwani Unguja na Pemba, sauti ya 'b' ni [ɓ] (isipokuwa baada ya sauti [m] isiyokuwa silabi itakuwa [b]), katika makala hii hatutumii ishara za kifonetiki. Sauti za 'd', 'g' na 'j' ni sawa.

<Picha ya 1> Buibui (spider; buibui/buibui, bui/bui)




<Picha ya 2> Funza (flea: funza/funza)




Kutokana na picha ya 1 mpaka 4, tunaweza kufahamu kuwa kila msamiati una maneno mbalimbali. Na kutokana na matokeo ya utafiti huu, haiwezekani kusema kama ‘neno hili alilitaja mtu aliye na umri fulani’ ama ‘neno lile alilitaja mtu aliye na jinsia hii’ n.k. Lakini inasemekana kwamba hata mkazi wa ZT wazazi wake wote wawili au japo mmoja tu ni aliyezaliwa katika mkoa wa Kaskazini Unguja, alitaja maneno mamoja na mkazi wa WK. Hata hivyo, kutokana na picha hizo zote ni wazi kwamba wakazi wa WK vilevile hawakutaja maneno mamoja. Isipokuwa mfano wa ‘butterfly’ - waliotaja neno ‘t’unguja (umoja) / t’unguja (wingi)[15]’ au neno ‘kitunguja (umoja) / vitunguja (wingi)’ wazazi wao wote walizaliwa kisiwa cha Tumbatu - na mfano wa ‘dragonfly’ - waliotaja neno ‘kurumbizi (umoja) / kurumbizi (wingi)’ au neno ‘kurumbiza (umoja) / kurumbiza (wingi)’ wazazi wao wote walizaliwa kisiwa cha Pemba-, hakuna matokeo yanayotusaidia tufahamu vizuri hali hii ya kuwepo maneno mengi mbalimbali yanayomaanisha dhana moja.

[15] Alama ’ inaonyesha sauti iliyoko kabla ya alama hii inatamkwa pamoja na pumzi kali. Sauti za ‘p’, ‘t’, ‘k’ na ‘ch’ zinatamkwa na pumzi kali baadhi ya wakati, lakini kwa Kiswahili Sanifu hakitofautishi sauti hizi, katika kitabu kinachoeleza sarufi ya Kiswahili imeandikwa kama “kuna sauti za pumzi”, basi. Katika utafiti wa msamiati, imetokea kwamba kwa neno moja watu kadhaa wanatamka bila ya sauti ya pumzi, wengine wanatamka pamoja na sauti ya pumzi. Bado hatuna uhakika sababu yake inatokana na taathira za elimu hasa za kutumia Kiswahili Sanifu au la, ama, vijana tayari wameanza kubadilisha ‘msamiati wa lahaja’ au la.

<Picha ya 3> Kipepeo (butterfly; kipepeo/vipepeo, popo/popo)




<Picha ya 4> Kereng'ende (dragonfly; kereng'ende/kereng'ende)




Inasemekana kuwa vijiji vilivyoko katika WK vilijengwa na wanaotoka kisiwa cha Tumbatu, na tukiwauliza wahojiwa kwamba wanatumia Kiswahili gani kwa kawaida wengine wanajibu "Natumia Kitumbatu". Lakini kwa mujibu wa matokeo hayo hatuwezi kusema katika WK msamiati wa Kitumbatu unatumiwa bila ya tofauti yoyote na msamiati wanaotumia wakazi wa kisiwa cha Tumbatu.

### 2.1.2 Aina ya Matunda

Hapa tuangalie maneno mawili 'tomato' na 'mango'. Kwa kamusi ya Kiswahili Sanifu tunapata kwanza neno 'nyanya (umoja)/nyanya (wingi)' kwa maana ya 'tomato'. Bara hilo ni neno la kawaida tu, lakini visiwani Unguja na Pemba watu hawatumii neno hilo kwa sababu 'nyanya' ni

tunda tofauti kabisa kama 'nyanya chungu' wanaloita watu wa bara, ndilo tunda chungu sana. Watu wa Unguja na Pemba wanatumia neno 'tungule (umoja)/tungule (wingi)' ama neno 't'ungule (umoja) / t'ungule (wingi)'. Kutokana na picha ya 5 tumefahamu waziwazi kwamba wahojiwa wote hawatumii neno 'nyanya'. Ingawa kuna tofauti ya matamshi kama kutamka sauti za mpumuo au la, wahojiwa wote wanataja neno 'tungule'. Tokeo hili linaonyesha kuwa wahojiwa wa visiwani wanahifadhi msamiati kwa dhati. Kusema la kweli, wakati nilipotazama vizuri akina mama walipopika chakula jikoni huko kijijini Chaani, hawakutumia neno jingine isipokuwa 'tungule'. Mwanamke mmoja aliyezaliwa Chaani ambaye hivi sasa anayekaa mjini Tanga tangu alipoolewa, aliporudi Chaani na kusikia neno 'tungule' kutoka kwangu aliniambia, "wewe ndiye Mzanzibari hasa kuliko mimi kwa sababu siku hizi natumia neno 'nyanya' siyo 'tungule'. Kisa hiki pia kinaonyesha wazi tofauti ya msamiati baina ya bara na visiwani.

<Picha ya 5> Nyanya (tomato; nyanya/nyanya, tungule/tungule, tunguja/tunguja)




<Picha ya 6> Embe (mango; embe/maembe)




Ingawa neno 'mango' ni 'embe (umoja) / maembe (wingi)' kwa Kiswahili Sanifu, kutokana na matokeo ya utafiti huu, tumepata maneno tofauti kama yenye vokali nyingine mwanzoni mwa neno la umoja au maumbo mbalimbali ya neno la wingi. Halafu tukiangalia picha ya 6, kuna wahojiwa wanaotumia 'embe/maembe' kama Kiswahili Sanifu asilimia 40 hivi hasa huko ZT, lakini wengine wote wanatumia neno moja kwa umoja na wingi. Kutokana na jambo hilo, inawezekana kusema kwamba wakati Kiswahili Sanifu kilipotayarishwa msamiati wote wa aina za tunda ulihamishwa ngeli zake kutoka ngeli za kama 9/10 kwenda ngeli za 5/6 kwa kufuatana na neno la jumla 'tunda (umoja) / matunda (wingi)'. Juu ya swala hili utafiti mwingine wa dhati unahitajika.

### 2.1.3 Aina ya Viumbe wa Baharini

Hapa tuangalie maneno matatu ‘skate’, ‘starfish’ na ‘jellyfish’. Neno ‘skate’ ni ‘taa (umoja) / taa (wingi)’ kwa Kiswahili Sanifu. Neno ‘starfish’ ni ‘kiti cha pweza (umoja) / viti vya pweza (wingi)’ kwa Kiswahili Sanifu. Neno ‘jellyfish’ ni ‘kiwavi (wa baharini) (umoja) / viwavi (wa baharini) (wingi)’ kwa Kiswahili Sanifu. Neno ‘kiwavi’ lina maana ya ‘aina ya majani yanayowasha’ na ‘mdudu mwenye miguu mingi ambaye aghalabu huwa na manyoya yanayowasha’, kwa hivyo tukitaka kufafanua maana yake tunatia maneno ya ‘wa baharini’. Watu wa visiwani wanakula ‘skate’ kwa kawaida, kwa hivyo wahojiwa wote wanajua na wakajibu, lakini kuhusu ‘starfish’ na ‘jellyfish’ wengine hawajui ama walijibu “sijawahi kuona” isipokuwa wavuvi au wanaokaa katika vijiji vilivyoko pwani, basi idadi ya majibu si kubwa.

<Picha ya 7> Taa (skate; taa/taa)




Tukitazama picha ya 7, inafahamika kuwa nusu ya wahojiwa walijibu maneno sawasawa na ya Kiswahili Sanifu au maneno sawasawa yenye tofauti ya sauti (mfano: kuna sauti ya pumzi, baina ya vokali inatokea nusu vokali, n.k.). Msamiati tofauti kabisa ni ‘katwe (umoja) / katwe (wingi)’ au ‘k’atwe (umoja) / k’atwe (wingi)’. Maneno haya yalitajwa na wahojiwa ambao wazazi wao wote wawili wanatoka Kusini mwa kisiwa cha Unguja. Na msamiati mwingine tofauti kabisa ni ‘nyenga (umoja) / nyenga (wingi)’ au ‘nyenga (umoja) / manyenga (wingi)’. Maneno haya yalitajwa na wahojiwa ambao wazazi wao wote wawili au mmoja anatoka kisiwa cha Tumbatu ama Kusini mwa kisiwa cha Pemba. Kutokana na haya, inawezekana kukisia kuwa msamiati wa samaki wanaoonekana mara nyingi kwa kawaida kila sehemu inayo maneno maalum na msamiati kama huo haubadiliki kirahisi hata ukipata taathira ya lahaja au lugha nyingine.

Tukiangalia picha ya 8, tunavutiwa na neno linalomaanisha ‘octopus’ kuliko maneno yanayomaanisha ‘starfish’ yenyewe. Wahojiwa wengi, kiasi asilimia 70 hivi walitaja neno sawasawa na Kiswahili Sanifu, lakini wako wawili waliotaja neno ‘nyambo’ badala ya ‘pweza’ kwa

kumaanisha ‘octopus’. Wahojiwa hawa wawili, wazazi wao wote wanatoka kisiwa cha Tumbatu[16].

<Picha ya 8> Kiti cha pweza (star fish; kiti cha pweza/viti vya pweza)




<Picha ya 9> Kiwavi (jellyfish; kiwavi/viwavi)




Neno ‘jellyfish’, tukitazama picha ya 9, lina maneno ya aina mbalimbali kama neno ‘butterfly’ na ‘dragonfly’, lakini wahojiwa waliojibu neno sawasawa na Kiswahili Sanifu ni chini ya asilimia 20. Neno ‘konyeza’ linatuonyesha ‘rangi kali ya kienyeji’, wahojiwa waliotaja neno hili wazazi wao wote au mmoja anatoka kisiwani Pemba. Halafu, maneno ‘kohoo la p’ap’a’ hayakutajwa kabisa na wahojiwa ambao wazazi wao wote wanatoka Kusini mwa kisiwa cha Unguja, bali wahojiwa wengi walitaja, kwa hivyo inasemekana kuwa maneno haya ni ya kawaida tu Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja. Neno ‘kohoo’ maana yake ni ‘sputum’, kwa hivyo hao wanaita ‘jellyfish’ ni ‘sputum of shark’ ama ‘sputum of ocean’.

[16] Na isitoshe, neno hili ‘nyambo’ au neno ‘nambo’ ambalo linatofautiana na sauti ya kwanza tu, lilitajwa na wahojiwa huko kisiwa cha Lamu, cha Pate, cha Siu nchini Kenya. Uhusiano huo ni swala litakalohitajiwa kuzingatia siku za mbele.

### 2.1.4 Muhtasari

Inasemekana kwamba ndani ya ZT na ndani ya WK zipo tofauti nyingi za msamiati na pahala pote pawili panahifadhi vizuri msamiati wake kuliko ilivyokisiwa kabla ya kufanya utafiti, haikuwa kama msamiati wa wakazi wa ZT ni sawasawa na wa Kiswahili Sanifu na msamiati wa wakazi wa WK ni sawasawa na wa Kitumbatu. Kama tulivyoonyesha juu, sababu ya kutokea tofauti kubwa kama hivi zinakisiwa kuwa kuna taathira za walipozaliwa wazazi wa wahojiwa, msamiati wenyewe unatofautiana baina ya bara na visiwani, au lahaja fulani ina msamiati maalum usio sawasawa na wa halaja nyingine, n.k., lakini kwa vyovyote vile, kutokana na matokeo ya kwamba hata katika kijiji kimoja tumepata majibu mbalimbali ya msamiati, inawezekana kusema kuwa kwa upande mmoja baadhi ya msamiati wa lahaja fulani umehifadhiwa kwa makini sana lakini kwa upande mwingine msamiati mwingine unapata taathira za lahaja/lugha nyingine na kubadilika. Kuna neno linalotumiwa huko bara kwa kawaida lakini lisilotumiwa katika WK wala ZT ambapo watu wengi wanaingia na kutoka, na kuna neno linalotumiwa katika vijiji vya WK lakini si sawasawa na neno la Kitumbatu.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, haiwezekani kusema mara moja kwamba vijana ndio wanatumia maneno mapya au yaliyo tofauti kabisa na ya kiasili, lakini siku za mbele idadi ya wazee wanaohifadhi maneno ya kiasili ikipungua kidogokidogo, na tena kwenda na kurudi watu huko bara kukizidi, inazewekana kutokea hali kama mabadiliko ya maneno yatapata kasi zaidi kuliko sasa[17)].

## 2.2 Hali ya Kuwasiliana Lahaja: Kutokana na Utafiti juu ya Mipaka Inayoruhusiwa ya Kufanya Ndoa

Sasa tuangalie kama lahaja moja na nyingine zinawasiliana vipi. Hapa tuhakikishe kama 'mipaka inayoruhusiwa ya kufanya ndoa' na 'mabadiliko ya lugha' yanahusiana au la na ikiwa kweli yanahusiana ni kwa kiasi gani / yanahusiana vipi kwa kutumia matokeo ya utafiti wa kuwahoji wakazi wa vijiji vinane vya WK - Nungwi (NG), Chaani (CH), Kidoti (KD), Matemwe (MT), Mkokotoni (MK), Kibeni (KB), Mkwajuni (MJ), na Gamba (GB) - kwa kutumia maswali ya jedwali la 1.

---

17) Wakati nilipofanya utafiti mwaka 1998, boti ilikwenda na kurudi mara tano kwa siku baina ya kisiwa cha Unguja na Dar-es-Salaam, na kulikuwa na boti au ndege ya kwenda na kurudi Tanga, Mombasa nchini Kenya mara kadhaa kwa siku, kwa hivyo watu wengi walikuwa wanakwenda na kurudi sehemu nyingine. Katika ZT imekuwa si adimu kuwaona watu wa bara, na kinyume chake, watu wa visiwani pia wengi wamekwenda Dar-es-Salaam. Waliozaliwa ZT na kukua pia ZT hasa wenye umri wa miaka 50 au zaidi waliniambia kuwa "siwezi kufahamu lugha wanayosema vijana wa siku hizi, lugha yao mbaya sana", "vijana wa siku hizi hawasemi Kiswahili fasaha cha Kiunguja-Mjini". Basi ni lazima tuzingatie hali halisi ya matumizi ya lugha hasa ya vijana wa ZT.

Kwanza, jedwali la 3 limeonyesha umri na jinsia ya wahojiwa wote. Kwa mfano ‘20M’ maana yake ni ‘wahojiwa wa kiume wenye umri wa miaka 20 mpaka 29’, na ‘10F’ maana yake ni ‘wahojiwa wa kike wenye umri wa miaka 10 mpaka 19’. Na majina ya vijiji yameonyeshwa kwa kifupisho. Halafu katika picha ya 10 imeonyeshwa kuwa wahojiwa wanatumia lahaja gani ya Kiswahili na wenzi wao (yaani mke au mume wa mhojiwa) wanatumia lahaja gani ya Kiswahili kwa kawaida. Kutokana na picha hii ya 10 tumefahamu kuwa wahojiwa zaidi ya asilimia 60 wanatumia lahaja moja na wenzi wao, na lahaja wanayotambua wahojiwa kwamba ‘hii inatumika wanapokaa’ wanaiita ‘Kiswahili cha wanapokaa’, kwa mfano kwa wakazi wa NG ni Kiswahili cha Nungwi. Lakini, kijijini MK, ambapo ni kiungo cha kwenda na kurudi kisiwa cha Tumbatu, wako wengi waliohamia kutoka sehemu nyingine na wafanya kazi katika ofisi za kiserikali, basi matokeo yake ni tofauti kabisa na ya vijiji vingine.

<Jedwali la 3> Umri na jinsia ya wahojiwa

| | 20M | 30M | 40M | 50M | 60M | 90M | 10F | 20F | 30F | 40F | 50F | 60F | 70F | 80F | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NG | 4 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 20 |
| CH | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 3 | 3 | 4 | 1 | 0 | 1 | 20 |
| KD | 3 | 3 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 6 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 20 |
| MT | 7 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 4 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 20 |
| MK | 0 | 7 | 4 | 2 | 5 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 |
| KB | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 | 1 | 3 | 6 | 3 | 2 | 1 | 1 | 0 | 22 |
| MJ | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 | 4 | 5 | 1 | 21 |
| GB | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 5 | 2 | 2 | 2 | 4 | 0 | 1 | 20 |
| Jumla | 17 | 17 | 10 | 4 | 10 | 1 | 3 | 27 | 22 | 13 | 13 | 10 | 7 | 3 | 163 |

Na ikiwa ni wahojiwa wa kike, hata wanaotoka sehemu nyingine ama kijiji kingine, kawaida hawahifadhi lahaja ya walikozaliwa bali wametanabahi kuwa wameshabadilisha lugha ya kutumia kila siku iwe lahaja ya wanakokaa baada ya kuolewa. Hii imehakikishwa kwa majibu ya wahojiwa wa kike wanaotoka sehemu nyingine/kijiji kingine au wahojiwa wa kiume walio na wenzi wanaotoka sehemu nyingine/kijiji kingine kama vile “Situmii tena lahaja niliyotumia zamani” (mhojiwa wa kike), “Mke wangu amesahau Kiswahili cha kijiji alikozaliwa” (mhojiwa wa kiume). Lakini kusema la kweli wanawake kama hao si wengi sana. Kwa sababu, tukiangalia picha ya 11 inayoonyesha sababu za kuoana tufahamu mara moja, idadi ya wahojiwa waliooana na watu wasio ndugu au wanaotoka sehemu nyingine ni chini ya asilimia 3.

Kutokana na matokeo hayo tunaweza kusema kama hivi:

1) Mipaka inayoruhusiwa ya kufanya ndoa kawaida imewekwa ndani ya kijiji kimoja na hata ikipanuliwa, hadi kijiji kilichoko karibu ambako ndugu wanaishi.

2) Kwa hivyo nyumbani lahaja moja na nyingine hazikutani kwa kawaida na haitokei hali ya kutumia lahaja mbili kwa mchanganyiko.

3) Kwa sababu ya 1) na 2), lahaja ya kijiji hicho inaweza kuhifadhiwa.

<Picha ya 10> Uhusiano wa lugha inayotumiwa baina ya wahojiwa na wanzao




<Picha ya 11> Sababu ya kuoana na mwenzi



Sasa tuangalie kama wahojiwa wanaona kwamba lahaja zao wenyewe zinahifadhiwa au la. Na tena tuangalie kama kwa kweli lahaja zao zinahifadhiwa au la. Kutokana na matokeo ya swali la 5 la jedwali la 1, katika wahojiwa 146 wenye watoto asilimia 92.5 hivi yaani wahojiwa 135 wamejibu "lugha yangu mwenyewe na lugha anayotumia mwanangu hazitofautiani". Kwa hivyo, kwa maoni yao wenyewe inasemekana kuwa hata kizazi kikibadilika lahaja haibadiliki kwa ghafla. Na katika utafiti wa mtazamo juu ya lugha, kwa swali la 13 la jedwali la 2, wahojiwa 21 wa CH (idadi ya wahojiwa wote ni 25) wamejibu kwamba lahaja yao itahifadhiwa, na wahojiwa 19 wamejibu kwamba 'lugha/lahaja wanayotaka mtoto wao atumie' ni 'lahaja ya wanapokaa' yaani 'Kiswahili chao wenyewe'. Kutokana na matokeo hayo, wengi wanaosema lahaja zao wenyewe hawana maoni ya kuzichukua lahaja zao kuwa lugha ya kiwango cha chini, wala hawahisi hatari ya kubadilika lugha zao wenyewe.

Lakini, ingawa wako wachache sana, wahojiwa wengine wamejibu kama hivi: "lahaja anayotumia mwanangu imeanza kutofautiana na yangu mimi kwa sababu anasoma Kiswahili kingine shuleni", "watoto wanaokaa ZT sasa wanasema lahaja ya mjini, hawasemi hata lahaja ya kijijini". Inasemekana kuwa 'Kiswahili cha shuleni' ni Kiswahili Sanifu ambayo ni lugha ya kielimu, na 'lahaja ya mjini' ni Kiunguja-Mjini. Wahojiwa wanaojibu kama hivi wametanabahi kuwa lahaja zao wenyewe zimepata taathira fulani za Kiswahili Sanifu ama Kiunguja-Mjini.

Kwa kweli tumepata taswira inayotofautiana sana na maoni ya wahojiwa wengi kwa kuchunguza kwa makini mazungumzo ya kawaida ya wanakijiji. Baina ya Kichaani anachoongea mzee mwenye umri zaidi ya 70 na Kichaani anachoongea kijana mwenye umri wa 10 na kitu, zimeonekana tofauti za kisarufi na kimsamiati[18]. Asilimia 90 ya vijana wa CH wanakwenda japo

[18] Natoa mifano kadhaa juu ya tofauti za kisarufi na kimsamiati baina ya mzee (A) na kijana (B) huko CH.
(1) Sikukiona.
A: Sechona. (Si-e-ki-on-a: 1sgNgSM-PstNg-OM7-see-BF)
B: Sikuchona. (Si-ku-ki-on-a :1sgNgSM-PstNg-OM7-see-BF)
(2) Mvua inanyesha.
A: Vuya inakunya. (vuya: rain9, i-na-ku-ny-a: SM9-Pres-Inf-rain-BF)
B: Mvua inanyesha. (mvua: rain9, i-na-nyesh-a: SM9-Pres-rain-BF)
(3) Umekula chakula cha mchana?
A: Kushakulya (ku-sha-ku-ly-a: 2sgSM-Peft-Inf-eat-BF) vitu vya mchana (vitu: thing 8, vya: of 8, mchana: noon) ?
B: Umekula (u-me-ku-l-a: 2sgSM-Peft-Inf-eat-BF) chamchana (chamchana: lunch 7) ?
Nimefanya utafiti wa kiisimu wa Kichaani na lahaja nyingine za WK tangu mwaka 1997 na ninaendelea hivi sasa mnamo mwaka 2018. Nimeandika makala kadhaa juu ya sarufi na msamiati wa hasa Kichaani, Kidoti, Kitumbatu-Gomani. Uangalie marejeo kama 竹村 (2013, 2014) na Takemura (2015, 2016, 2017).
Na Whiteley (1956) aliandika makala yake ya kiisimu juu ya Kimtang'ata (Whiteley alieleza hiki ni kilahaja cha kusini cha Kimrima kinachozungumzwa kutoka Shimoni kwa kaskazini mpaka Sadani kwa kusini), tukisoma makala hii tunafahamu kuwa sentensi za wakati uliopo za Kimtang'ata na Kichaani zinafanana sana kwa kutokea nakala za vokali mwishoni mwa vitenzi. Na tena Whiteley alisisitiza kuwa msamiati wa Kimtang'ata unatofautiana na wa Kiunguja-Mjini, bali unafanana zaidi na wa Kipemba. Basi inasemekana kuwa unahitajika utafiti mpana/wa kina zaidi wa kisarufi wa Viswahili vya mwambaoni mwa Tanzania Bara

shule ya msingi, yaani wanasoma sarufi ya Kiswahili Sanifu katika darasa la Kiswahili na masomo mengine pia wanasoma kwa Kiswahili rasmi. Haiwezekani kusema mara moja kwamba Kiswahili cha vijana kimeanza kuwa kama Kiswahili Sanifu, lakini hata hivyo, haisemekani kuwa lahaja ya sehemu fulani imehifadhiwa kikamilifu, bali inaeleweka kuwa kumetokea mabadiliko ya lahaja kidogokidogo hali inayopingana na maoni ya wahojiwa.

Kwa swali la 6 la jedwali la 1, wahojiwa asilimia 60 hivi wamejibu kama "zamani wazazi waliamua mchumba wa mwana wao kuwa ndugu kwa ndugu au jirani kwa jirani, ilikuwa adimu sana kuruhusiwa kuoana na mtu anayetoka sehemu nyingine, siku hizi tuko huru kwenda na kurudi pahala popote na wazazi wenyewe hawatukatazi sisi kupendana na yeyote, basi tunaweza kupendana na kuoana na yeyote anayetoka popote". Lakini tumefahamu hali yenyewe ni kinyume na jibu hilo kwa sababu mipaka inayoruhisiwa ya kufanya ndoa haijapanuliwa kama tulivyoona juu. Kwa hivyo, inasemekana kuwa mabadiliko ya lahaja fulani hayapati taathira za 'kuoana watu', bali yanaathiriwa zaidi na upanuzi wa njia za usafirishaji na uhuru wa kwenda na kurudi pahala pengine popote. Mhojiwa mmoja alieleza sababu ya kuongezeka kwa idadi ya watu kwenda Tanzania bara au sehemu nyingine kama hivi: "kwa mujibu wa mabadiliko ya kisiasa, baada ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, ulifutwa ubaguzi juu ya watu wa bara na tulipata uhuru wa kwenda bara". Sasa hasa vijana wanatamani sana kwenda nje ya vijiji vyao na wanahitaji kupata uwezo wa kutumia lugha ya mawasiliano kama Kiswahili Sanifu ama Kiunguja-Mjini.

### 2.3 Thamani ya Lahaja na Kiswahili Sanifu: Kutokana na Utafiti wa Mtazamo juu ya Lugha

Kwa mujibu wa kazi ya kiisimu-jamii inaelezwa kuwa "kila mtu ana uwezo wa kuzungumza lugha au lahaja kadhaa si moja tu kwa kawaida, basi ni uwezo wa kawaida tu kwa binadamu kutumia na kufafanua lahaja kadhaa za lugha moja" (シュリーベン=ランゲ 1990:120). Kusema la kweli, katika kila utafiti tumepata majibu mengi ya kuwa "lugha ninayoweza kuzungumza si moja bali ni nyingi". Nimetaja katika makala yangu nyingine kwamba tofauti za uwezo wa 'kuzungumza lahaja moja tu' mpaka wa 'kuzungumza lahaja au lugha nyingi' zinasababishwa na kuwahi kusoma au la, kuishi wapi na kuwahi kuhama au la (竹村 1999:12). Sasa, tuangalie kwa makini wahojiwa wenye uwezo wa kuzungumza lahaja kadhaa wanazithamini kwa zamu au vipi, yaani wanaziona lahaja hizo kama "hii ina kiwango cha juu zaidi", "hii ina kiwango cha chini kabisa", n.k. kutokana na matokeo ya swali la 11 la jedwali la 2 na ya swali la 8 la jedwali la 1.

Kuhusu swali la 11 la jedwali la 2, wahojiwa 13 wa CH (kwa jumla wahojiwa 25) walitoa jibu la kuithamini vizuri lahaja ya Kiunguja-Mjini. Sababu zake ni kama "ni lugha anayofahamu yeyote",

---

pia.

“matamshi yake yanatupendeza kuliko ya kishamba”, “kwa kutumia Kiunguja-Mjini tunaweza kuwasiliana na yeyote anayetoka popote”, “hata mimi natumia Kiunguja-Mjini huko mjini”, n.k. Wahojiwa waliojibu wengi wana umri wa kuanzia 30 mpaka chini ya 50, hawa wanakwenda mjini kufanya kazi au walipata elimu zao za kati na juu huko mjini. Halafu kuhusu swali la 8 la jedwali la 1, idadi ya wahojiwa waliojibu “Najua” ni 54, na katika hao wahojiwa 53 walisema kuwa “lazima natumia lugha hii mjini/lazima naiga kusema lugha hii”. Kwa matokeo hayo inasemekana kuwa wakazi wa WK wanafikiria ZT ni ‘jiji’ ambalo wako watu wengi mno wanaotoka sehemu mbalimbali, basi huko wanatakiwa watu wote wazungumze Kiunguja-Mjini. Na wakazi wa ZT bila shaka wanaithamini lahaja yao, wahojiwa zaidi ya asilimia 90 walisema maoni ya kuthibitisha thamani yake kwa mfano “Kiunguja-Mjini ni lugha nzuri zaidi na ya kupendeza Afrika ya Mashariki”, “ni lugha ya mawasiliano kwa watu wote”, “hata anayetoka shamba hata anayetoka nchi ya nje anaweza kufahamu lugha hii kirahisi, na tena inatumiwa shuleni, benki, ofisini, na sehemu nyingine za kirasmi”. Baadhi yao wanatoka sehemu nyingine siyo ZT, na wahojiwa kama hao wanazithamini lahaja zao na kuziweka umuhimu kwa kutoa maoni kama “lahaja yangu ni ya nchi yangu, ya wazazi wangu, basi ni muhimu sana”, “naisifu lahaja yangu kama najisifu mwenyewe, lahaja zote ni za asili ya Kiswahili Sanifu kwa hivyo lazima tuzihifadhi”.

Lakini, hali halisi ya kutumia lahaja za Kiswahili haiendani na maoni yaliyotajwa ya kuzisifu lahaja. Wahojiwa wengi wanawataka watoto wao waliozaliwa ZT watumie lahaja ya ZT yaani Kiunguja-Mjini, hawajitahidi wala hawazingatii kuwalazimisha watoto wao watumie lahaja za kwao. Na isitoshe, wahojiwa waliozaliwa na waliokulia ZT wanaona kuwa “hapa ZT yeyote anatakiwa kutumia Kiunguja-Mjini na kadri nijuavyo hata watu wanaotoka popote pale wanatumia hicho. Ikiwa watatumia lahaja za shamba kwa ukaidi, itasababisha tatizo ama balaa kwa kuzalisha hali ya kutosikilizana”.

Kutokana na matokeo yaliyotajwa juu, inafahamika kuwa ZT ingawa ni ‘jiji’ dogo sana lakini watu wengi wanakusanyika hapo kutoka sehemu mbalimbali na unakuzwa uchumi wake na njia za usafirishaji zinapanuka, kufuatana na hali hiyo lahaja ya ZT yaani Kiunguja-Mjini kinapata thamani kubwa zaidi kuliko lahaja nyingine za kisiwani. Na tena, wahojiwa waliojibu kuwa Kiswahili Sanifu ni Kiunguja-Mjini wako si wachache, katika utafiti wa mipaka inayoruhusiwa ya kufanya ndoa wako kiasi asilimia 36, katika utafiti wa mtazamo juu ya lugha wako asilimia 40 (wahojiwa wa CH na ZT kwa jumla), na wako asilimia 64 (wahojiwa wa ZT peke yake). Hawa walisifu Kiswahili hiki kwa kusema kama “yeyote akisikia Kiswahili hiki atafahamu mara moja, hakina maneno matusi”, “siku hizi Kiswahili hiki kinatumika si mwambaoni tu bali katika sehemu nyingi sana, istilahi nyingi zimeshatayarishwa na cheo chake kimekuwa kikubwa zaidi kuliko zamani, ni lugha ya kupendeza hasa”, “ni lugha inayosifiwa na kuthaminiwa kitaifa ambayo watu wengi wanatumia”. Hali hii inaonyesha kwamba wako watu wanaotambua Kiunguja-Mjini ni lahaja ya juu kuliko lahaja

nyingine zote na tena watu kama hao si wachache bali wengi, na kutambua hivi hakuhusiani na kujua kuwa Kiunguja-Mjini ni msingi tu wa Kiswahili Sanifu si lugha moja.

### 3. Hitimisho: Taathira ya Kiswahili Sanifu na Siku za Mbele za 'Lahaja'

Kwa kujumuisha yaliyotajwa juu, inawezekana kusema kwamba lahaja za Kiswahili isipokuwa Kiunguja-Mjini zitabadilika kwa kuathiriwa na Kiswahili Sanifu ama Kiunguja-Mjini, na wasemaji-lahaja wakitaka wasitake lahaja zao zitamezwa na lahaja ya kiwango cha juu zaidi.

Kwa mfano kama ikitokea kesho tu wasemaji wa Kichaani waache lahaja yao na kuanza kutumia Kiunguja-Mjini basi Kichaani kinaweza kufutika kabisa, lakini mabadiliko ya lugha hayatokei kama hivyo. Ikiwa lugha mbili zinatumiwa pamoja na lugha moja ina nguvu zaidi ya kijamii kuliko nyingine, mabadiliko ya lugha yatakuwa hivi: kwanza lazima lugha zote mbili zinatumiwa pamoja kwa muda, halafu lugha yenye nguvu zaidi ya kijamii inapanuliwa vipengele vya kutumiwa kidogo kidogo, mwishowe inatawala vipengele vyote.

Lakini haitakuwa kama "lahaja zote zinakufa kabisa". Kwa mfano juu ya lahaja za Kijapani imeanzishwa dhana ya 'lahaja mpya'[19] (安田 1999:327-328), inayomaanisha 'lahaja ambayo imebadilika kwa kupata taathira za lugha sanifu'. Hii dhana bila shaka inatumika kwa lahaja za Kiswahili pia. Kiswahili Sanifu ni Kiswahili kinachofikiriwa kutumiwa kirasmi katika elimu, vyombo vya mawasiliano, siasa, uchumi, n.k. katika kiwango cha kitaifa kama tulivyotaja juu tayari. Lakini Kiswahili hiki kilitayarishwa na Kamati ya Lugha (Kiswahili) ya Makoloni ya Uingereza miaka karibu 90 hivi iliyopita, na baada ya Tanzania kupata uhuru, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam ilidumisha kanuni ya uandishi, matamshi na sarufi. Hata hivyo, haiwezekani kutumiwa kila pahala kwa kufuata kanuni hiyo kuwa lugha ya mfano mzuri. Aidha, katika mazungumzo ya kawaida, hata Kiswahili Sanifu vilevile kinaathiriwa na lahaja nyingi nyinginezo zinazosababishwa na pahala, elimu, kazi, n.k., hata mtu fulani akijiona "mimi nazungumza Kiswahili Sanifu" katika mkusanyiko wa kirasmi, hicho anachokizungumza kina aina mbalimbali tangu 'Kiswahili kinachokaribiana zaidi na Kiswahili Sanifu' mpaka 'Kiswahili kinachokaribiana zaidi na lahaja fulani'.

Inasemekana kuwa lahaja zilizochambuliwa zamani kwa kufuatana na 'sehemu' kama Unguja-Mjini, Chaani, Tumbatu, n.k. zinaonyesha upande mmoja tu wa lahaja, niseme kama ni 'lahaja za wazee'. Vijana hasa wanaokwenda au waliowahi kwenda shuleni wameanza zamani kusema 'lahaja mpya', na isitoshe hizi lahaja mpya zenyewe zina aina mbalimbali kwani hizi ni mchanganyiko wa lahaja fulani na Kiswahili Sanifu na kiasi cha kuchanganyika kinatofautiana kwa

[19] Kiasili hii dhana ya 'lahaja mpya' ilianzishwa na Sanada Shinji. Alieleza makini katika kitabu chake kinachoitwa *Chiikigo no Dynamism* (Nguvu za Lugha za Kienyeji), おうふう, 1996.

mujibu wa msemaji-lahaja mpya amepata elimu gani, anajua Kiswahili Sanifu kiasi gani, na anatumia lahaja yake ya alikozaliwa kwa kiwango gani. Hatuna uhakika kuwa siku za mbele nchini Tanzania itasisitizwa sera ya kukikuza Kiswahili Sanifu au la, lakini imefahamika kuwa dhima yake Kiswahili Sanifu ni 'kuunganisha wananchi', basi vipengele vyake vya matumizi havitapunguzwa, bali vitapanuliwa zaidi. Na hata wasemaji wa lahaja za Kiswahili kama lugha zao mama watajitahidi kusema au kuiga kusema Kiswahili Sanifu ili wapate faida zaidi ya kijamii na kiuchumi. Kwa sababu ya mkondo kama huo, 'lahaja mpya' zitazaliwa zaidi na zaidi na kusikika katika vipengele vingi zaidi kuliko hivi sasa.

Lakini hata hivyo hatuwezi kufafanua mara moja "tukizungumza hivi ndio usemaji wa Kiswahili Sanifu" ama "tukizungumza hivi ndio usemaji wa lahaja ya pahala fulani" kama tunavyojibu maswali kitakwimu. Hata 'mtu mmoja' akizungumza, lugha yake anayozungumza inawezekana kubadilika kwa kutegemea "yeye ndiyo <nani>", "anazungumza <wapi>", "anazungumza <na nani>", na vilevile inazewekana kuchanganyika lugha/lahaja zaidi ya mbili. Kama tulivyotaja juu, wakazi wa WK wana maoni ya kuwa lahaja zao walizozaliwa nazo hazifutwi na lahaja/lugha nyingine yoyote. Kadri wawezavyo kuhifadhi maoni kama hayo, 'lahaja ya pahala fulani' haifutiki katika lugha anazotumia mtu fulani kibinafsi. Kwa jumla tuseme kwamba hatujawahi kufafanua wala kuchambua hali halisi ya Kiswahili chenyewe, basi lazima tuangalie kwa makini maendeleo ya kuwepo Kiswahili ambacho ni mfululizo wa lahaja nyingi, ili kupata ufafanuzi juu ya tofauti na mwachano (diversity) uliomo katika 'lugha moja'/aina za vilugha vilivyomo katika lugha moja.

## Marejeo


カルヴェ, ルイ=ジャン. 1996.『超民族語』(林正寛訳). 白水社.

イ・ヨンスク. 1996.『「国語」という思想―近代日本の言語認識』. 岩波書店.

宮本正興. 1982.「現代スワヒリ語の性格―標準語の創造―」『民博通信』第 18 号. pp.31-139. 国立民族学博物館.

――. 1989.『スワヒリ文学の風土』. 大阪外国語大学アフリカ研究室.

――. 1990.「文字と文明―アフリカからの発想」『ことばの比較文明学』(梅棹忠夫・小川了編). pp.21-58. 福武書店.

長志珠絵. 1998.『近代日本と国語ナショナリズム』. 吉川弘館.

ロメイン, スザーン. 1997.『社会のなかの言語』(土田滋・高橋留美訳). 三省堂.

シュリーベン=ランゲ, ブリギッテ. 1990.『社会言語学の方法』(原聖・糟谷啓介・李守訳). 三元社.

竹村景子. 1993.「多民族国家における国家語の役割―タンザニアのスワヒリ語の場合―」『スワヒリ＆アフリカ研究』4:34-99. 大阪外国語大学スワヒリ語・アフリカ地域文化研究室.

――. 1999.「「方言」と「標準語」―スワヒリ語話者の言語意識調査から―」『アフリカ研究』55:1-20.

――. 2013.「スワヒリ語諸変種記述調査報告（2）―キベニ変種およびキドティ変種基礎語彙 600 語―」『スワヒリ＆アフリカ研究』24:50-72.

――. 2014.「スワヒリ語チャアニ変種の接続形と命令形概観」『スワヒリ＆アフリカ研究』25:120-129.

安田敏朗. 1999.『〈国語〉と〈方言〉のあいだ―言語構築の政治学』. 人文書院.

Chum, Haji. 1994. *Msamiati wa Pekee wa Kikae*. Helsinki University Printhouse.

Maganga, Clement. 1983. 'Juhudi za Ukuzaji wa Kiswahili Tanzania Bara' *Malaka za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1- Lugha ya Kiswahili.* pp.93-105. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mazrui, Ali A. & Mazrui, Alamin M. 1995. *Swahili State and Society : The Political Economy of an African Language.* East African Educational Publishers.

Mkude, Daniel J. 1983. 'Mtawanyiko wa Lahaja za Kiswahili' *Malaka za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1- Lugha ya Kiswahili.* pp.62-83. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nurse, D. & Hinnebusch, T. J. 1993. *Swahili and Sabaki: A Linguistic History.* University of California Press.

Takemura, Keiko. 2015. 'Miundo ya Dhamira Matilaba na Dhamira Amri katika Kichaani' *Swahili & African Studies*. 26:170-180.

――. 2016. 'Miundo ya Sentensi zenye Kitenzi '-wa' katika Kichaani - Kwa Kulinganisha na Kiswahili Sanifu -' *Swahili & African Studies*. 27:53-63.

――. 2017. 'Miundo ya Sentensi za Njeo Iliyopita katika Kitumbatu-Gomani: Kwa Kulinganisha na Kichaani na Kiswahili Sanifu' *Swahili & African Studies*. 28:109-121.

Whiteley, W. H. 1956. *KI-MTANG'ATA: A Dialect of the Mrima Coast – Tanganyika.* East African Swahili Committee, Makerere College, Kampala.